

BUILDERS OF FUTURE AFRICA

Plot #2773, Lenjani village, 2km Up Hill from Habari Maalum, P.O.BOX 15170 Arusha, Tanzania.
Mob +255 767 544 371, +255 629 017 000, website: www.bfatanzania.org Blog: bfatz.ml/blog,
E-mail: info@bfatanzania.org



TAMKO LA KULAANI MAUJI YA MTOTO NOELA ASIMWE NOVARTH MWENYE ULEMAVU WA NGOZI (UALBINO) WA MKOANI KAGERA.

UTANGULIZI

Mnamo tarehe 30/5/2024 iliripotiwa kupotea kwa mtoto Noel Asimwe Novarth (17) ambae alikuwa akiishi na wazazi wake mkoani Kagera wilaya ya Muleba kijiji cha Bulamula, kisha kufuatia na habari mbaya ya kifo chake kilichotokana na kukatwa viungo vyake mbalimbali na mwili wake kutelekezwa kwenye daraja dogo (Karavati) iliyopo barabara ya Ruhanga Makongara ukiwa umewekwa kwenye mfuko wa sandalusi siku ya tarehe 17.6.2024. Habari hii kama ilivoripotiwa na vyombo mbalimbali vya habari, ni habari mbaya, ya kutisha na kusikitisha sana.

Sisi kama Shirika la Builders of Future Africa (BFA) tunalaani vikali tukio hili alilofanyiwa mtoto Asimwe kwa sababu tu ulemavu wake wa ngozi, tukio lenye kuleta sifa mbaya kwa nchi yetu na kutuondolea ustaarabu ulimwenguni. Tunaitaka serikali kuchukua hatua za haraka kufanya uchunguzi na kuwachukulia hatua kali kwa wote watakaobainika kuhusika kwa namna moja au nyingine juu ya kifo cha binti huyu mdogo.

Lakini pia, ni wakati muafaka kwa serikali yetu kuchukua hatua za zaidi za kiulinzi juu ya watoto na watu wote wenye ulemavu wa ngozi ili wajione salama kuishi kama watu wengine.

Ni ombi letu kwa wananchi wote kutoa ushirikiano kwa kuwafichua watu wote wanaohusika na kushamiri kwa vitendo hivi viovu.

Sisi kama BFA, tutaendelea kushirikiana na serikali na wadau wengine kutoa elimu, kulaani na aina nyingine za kuimarisha ulinzi kwa watoto na watu wenye ulemavu wa ngozi.

Imetolewa na Shirika la Builders of Future Africa (BFA)

Arusha, Tanzania

Tar 18.6.2024



[bfatanzania](https://www.instagram.com/bfatanzania)



[@bfatanzania](https://twitter.com/bfatanzania)



[@Builders of future Africa](https://www.facebook.com/BuildersoffutureAfrica)



info@bfatanzania.org



www.bfatanzania.org